**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima na afya njema inayotuwezesha kukutana hapa katika Mkutano huu wa Kumi na Tano ambao ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Aidha, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuongoza vyema, kutuelekeza na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mujibu wa Katiba na kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 na Mipango mikuu ya Maendeleo kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa dhati kabisa, kamati inatoa pongezi zake kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Ofisi hii lakini pia kusimamia utekelezaji wa

Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kupitia taasisi zote za Serikali na zisizo za Serikali kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi na kukuza demokrasia nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kukushukuru wewe binafsi kuweza kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako Tukufu kuweza kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa ***Bajeti kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi*** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na muelekeo wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wake, Dkt. Islam Seif Salum kwa utendaji mzuri wa kazi zake na ushirikiano mkubwa wanaoipatia kamati katika kutekeleza majukumu yake. Sambamba na hilo, napenda kuishukuru Ofisi hii kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 ambayo utekelezaji wake umefikia hatua kubwa sana ya mafanikio. Aidha, Ofisi imeweza kuwasilisha mwelekeo wa bajeti mpya kwa mwaka 2024/2025 ambapo pamoja na mambo mengine imeweza pia kuainisha vipaumbele vyote ambavyo msingi wake ni kuleta maendeleo chanya katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Wajumbe wa Kamati yangu

kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wao wa pamoja katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu, naomba sasa niwatambue wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdallah Abass Wadi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Panya Ali Abdallah | Mjumbe |

Aidha, kamati hii inaratibiwa kazi zake na makatibu watatu pamoja na mkalimani mmoja wa lugha za alama ambao wanatusaidia kutekeleza majukumu yetu kitaalamu na kiufanisi, Makatibu hao ni:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Ali Alawy Ali | - | Katibu |
| 2. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | - | Katibu, |
| 3. | Ndg. Shawana Mohammed Haji | - | Katibu, na |
| 4. | Ndg. Amina Abeid Hemed | - | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo naomba sasa kutoa maoni ya kamati yangu kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa bajeti hii kwa mwaka 2024/2025 kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ina mafungu matatu (03) ya kibajeti ambayo ni **fungu C01** Ofisi Kuu,

**fungu C02** Baraza la Wawakilishi na **fungu C03** Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Mafungu haya yanaendeshwa kwa progaramu Kuu na Programu Ndogo ambazo zimo katika kila fungu husika kama zilivyoainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kitabu cha Bajeti kuu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**,

Utekelezaji wa Programu hizi umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Mpango wa kukuza uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar, ahadi zilizotolewa na Viongozi Wakuu wa Nchi yetu, Hotuba mbali mbali na maagizo ya Mheshimiwa Rais ambayo anayoitoa kila anapopata fursa ya kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu kupitia **Program Kuu PC0101 ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** imeridhika na utekelezaji wa programu hii kwa namna ofisi ilivyojipanga na kusimamia malengo yake kwa muda wote wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na Bajeti Kuu ya 2023/2024. Hata hivyo, kamati haikuridhishwa na hali ilivyo kwa upande wa nyumba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili kwa upande wa Pemba kutokana na hali mbaya ya jengo lilisababishwa na uchakavu na hali mbaya ya ardhi iliyolizunguka eneo hilo. Vile vile, Kamati inaishauri ofisi kutatua changamoto ya usafiri pamoja na uhaba wa samani katika nyumba ya Mheshimiwa na ofisi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**,

Katika fungu **C01** Kupitia programu kuu ya ***Uratibu wa Shughuli za Serikali:*** Kamati kupitia programu ndogo ya **SC010201** ya Sherehe na

Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Kamati yetu inaipongeza Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa kusimamia vyema malengo yake na kuhakikisha yanaenda kama yanavyopangwa. Hata hivyo, Idara hii haifanyi vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya kila mwaka jambo ambalo limepelekea kupunguziwa kiwango cha makadirio ya mapato kutokana na uchache wa vyanzo vya mapato na kuchakaa kwa vifaa vyake wanavyotegemea kuwapatia kipato.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri kuongeza juhudi katika kuboresha vyanzo vya mapato ikiwemo milango ya maduka ya Mwanakwerekwe ambayo imechakaa na haiendani na wakati na mazingira husika. Kamati pia, inaishauri Serikali kuwapatia vifaa vya kisasa ambavyo vitaweza kufanya kazi kwa ushindani na wafanyabishara na jambo hili linawezekana kwani tayari limeainishwa katika mipango ya wizara kwa mwaka 2024/2025. Aidha, kamati inaishauri Serikali kupitia Idara ya Uratibu wa Serikali kuandaa muongozo utakaotumika katika maadhimisho ya sherehe za kitaifa ili kuondoa usumbufu unaojitokeza katika maandalizi ya sherehe za kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Sote tunavyofahamu kuwa suala la maafa katika jamii haliwezi kuepukika bali tunaweza kukabiliana nalo kwa namna linavyotokea kwa lengo la kupunguza athari za moja kwa moja kwa jamii. Kupitia programu ndogo ya **SC010201** ya Kukabiliana na Maafa. Kamati yangu inashauri Idara katika kutoa huduma na misaada ya maafa kuwepo uwiano ulio sawa katika jamii kwa kuzingatia maeneo mahususi. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya kukabiliana na maafa zinapatikana kwa madhumuni ya kutekeleza mipango yake pamoja na kuzisaidia jamii kujifariji wakati wa maafa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kujilinda na kukabiliana na maafa ambapo kwa mwaka wa 2023/2024 ulipangiwa fedha za uendeshaji za mradi kama hatua mbadala ya kupambana na maafa Zanzibar. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha kampeni maalumu ya kuanzisha mfuko wa kukabiliana na maafa Zanzibar kwa kuzingatia Sheria ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Nam. 1 ya 2015 na kanuni za maafa ambazo zinatumika kusimamia majanga mbali mbali katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa **Program Ndogo ya SC010204 ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha Muungano na kuondoa kwa kiasi kikubwa kero za Muungano. Aidha, kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu suala la nafasi za ajira za Muungano kwa kuwahamasisha vijana kuomba na kuzifanyia kazi. Kwa pamoja, tunazishauri taasisi zinazohusika na utoaji wa ajira za Muungano kwa upande wa Tanzania Bara, kushirikiana kikamilifu na taasisi za SMZ ambazo zina mchango mkubwa katika kufanikisha masuala ya ajira kwa upande wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaishauri Serikali kuimarisha huduma za uratibu wa shughuli za Serikali Dar es Salaam na Dodoma kwa kulipitia tamko lililoipa jina **Ofisi ya Uratibu SMZ Dodoma** na kusomeka **Ofisi ya Uratib SMZ Tanzania Bara**, mabadiliko ya jina hilo yatasaidia kujumuisha ofisi zote za uratibu zilizopo Tanzania Bara.

Sambamba na hilo, kamati inapendekeza kwa Serikali katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 kuweka kipaumbele katika ujenzi wa jengo jipya eneo la Mtumba ambalo tayari tumepatiwa kiwanja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kutanua wigo wa huduma katika Ofisi Kuu Dodoma kwa kupatiwa vyombo vya usafiri,

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia **Programu ndogo ya *Shughuli za SMZ*** ambayo inatekelezwa kupitia Mradi wa TASAF III kwa upande wa Zanzibar, Kamati inazipongeza Serikali zetu zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzidi kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha mradi huu ambao unasaidia sana wananchi wenye hali za chini katika kupunguza umasikini kupitia mradi wa Kaya Masikini.

Kipekee, kamati inawapongeza watendaji wa Makao Makuu Dodoma wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji TASAF Ndugu Shedrack Mzirai na watendaji wote wa Ofisi ya TASAF Zanzibar kwa kuwatumikia wananchi vizuri.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika ufuatiliaji wa shughuli zinazoratibiwa na TASAF, kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Upenja, mradi ambao unaendelea vizuri, ukumbi wa mikutano Bambi ambao tayari ujenzi wake umekamilika, sambamba na kufanya ziara katika Kijiji cha Chuini, ziara ambayo iliwakutanisha wanufaika wa mradi, ambapo walipata fursa ya kusikiliza changamoto zinazowakabili ambazo kiujumla zote zilipatiwa ufumbuzi na watendaji wa TASAF tulioongozana nao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kiujumla kamati imeridhika na hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa upande wa Zanzibar. Pamoja na kupitia programu hii kamati inashauri Serikali kuongeza uelewa kwa wananchi kutokana na malalamiko makubwa yanayojitokeza katika jamii wakati wa kutolewa katika mpango. Kamati inasisitiza kutolewa elimu ili wananchi wafahamu kuwa kuna sababu nyingi zinazopelekea mlengwa kutoka kwenye mpango pamoja na kupisha wengine ambao hawajaingia kwenye mpango huu ili nao wafaidike kwa kujikwamua na umasikini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa **Baraza la Wawakilishi yenye fungu C02,** kupitia programu ndogo ya **SC020201** Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi, Kamati imefarajika sana kuona jinsi mipango na mashauri mbali mbali yanavyotekelezwa siku hadi siku, na hivyo kupelekea kuimarika kwa dira na malengo ya Baraza ndani na nje ya Zanzibar.

Sambamba na hivyo, kamati inashauri, mpango wa ununuzi wa magari kwa ajili ya shughuli za kamati uweze kutekelezwa kwa vitendo kwani bado changamoto ipo katika suala zima la usafiri kwa Kamati za Baraza hasa wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za bajeti.

Kipekee, kamati inaishauri Afisi ya Baraza kuendeleza mpango wa ujenzi wa jengo jipya la Afisi ya Baraza ili kutatua changamoto ya nafasi kwa watendaji na waheshimiwa wajumbe.

**Mheshimiwa Spika**,

Katika **fungu C03 Tume ya Uchaguzi Zanzibar;** kupitia Programu Kuu **PC0302** ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za

Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa kazi zake nzuri na zenye manufaa kwa mustakbali wa kukuza demokrasia Zanzibar pamoja na kufanikiwa sana katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Mtambwe na Wadi ya Welezo. Mafanikio ya chaguzi hizi mbili ni mwangaza wa uchaguzi mkuu wa 2025 kuwa utakuwa wa huru na wa wazi ili kuonyesha ukomavu wa demokrasia hapa nchini.

Aidha, kamati inatoa pongezi kwa kupatiwa gari mpya 11 ndani ya mwaka huu wa 2023/2024 pamoja kuanza kwa ujenzi wa jengo jipya la Tume ambalo litaondosha kero ya uhaba wa nafasi kwa watendaji wa ofisi hiyo pamoja na kuweka miundombinu mipya kwa ajili ya chaguzi zijazo.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia Bajeti hii ya 2024/2025 Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati ili Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kukamilisha malengo yao. Kwani, kucheleweshwa kwa fedha za matumizi mengineyo kunapelekea watumishi kutolipwa stahiki zao mbali mbali kwa wakati na husababisha hali ngumu za maisha katika jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo waliyojipangia katika utekelezaji wa majukumu yao, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi na kwa niaba ya Kamati hii tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na wairidhie Bajeti hii na hatimae wapitishiwe mapato na matumizi ya fedha zote zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu **Naomba Kuunga Mkono Hoja.**

Ahsante,

……………………………

(Machano Othman Said)

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**<u>ZANZIBAR</u>**